AUSC
African Union Sports Council

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by:
giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

# Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake kupitia Michezo Afrika

# MAELEZO YA UTETEZI



# UTANGULIZI

Wasichana na wanawake kote Afrika wanaendelea kukumbana na matatizo na changamoto. Umoja wa Afrika unakusudia kupunguza vikwazo vikubwa katika usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake, kiasi kwamba wanawake na wasichana wanaweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kisiasa.

Ushiriki katika michezo unaweza kusaidia kuondoa fikra potofu za kijinsia huku ukiwawezesha wasichana na wanawake.

Michezo inatoa njia ya kibunifu ya kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia, kuondoa fikra na imani za kitamaduni ambazo zinzachochea uwepo wa taratibu zisizokuwa za haki na zenye madhara dhidi ya wanawake na wasichana Afrika na zaidi. Hadi sasa, mamilioni ya wanawake na wasichana bado wananyamazishwa na kunyimwa haki zao, zikiwemo haki za kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo kama njia ya kujenga afya, ushiriki wa kijamii na mafanikio ya michezo. Kuanzia ngazi ya juu hadi ya chini ya michezo, wanawake wanaendelea kuwa katika hali ngumu na wakati mwingine wanatengwa. Wanaume wa Kiafrika wanaocheza mpira wa miguu wanapata fursa za kujijenga kimaisha kama wachezaji wanaolipwa fedha nyingi, makocha, wamiliki wa vilabu na viongozi. Fursa za wanawake wa Kifrika wanaocheza mpira, kwa upande mwingine, zipo katika kiwango cha chini. Tofauti hizo zimeenea sana karibu katika michezo yote. Duniani, kwa kila saa 100 za michezo inayotangazwa katika televisheni, saa 4 tu zinatumika kutangaza michezo ya wanawake. Ingawa wanawake wanafikia hadi 40% ya washiriki wa michezo duniani, michezo ya wanawake inapata 1% tu ya ufadhili wa michezo. Wanaume ni wengi katika nafasi za ukocha kukiwa na kocha 1 kati ya makocha 5 wanaowafundisha wasichana na wanawake katika ngazi ya ushindani wakiwa wanawake.

# KUTOKUWA NA USAWA KATIKA MICHEZO: TAARIFA NA TAKWIMU

**Ukosefu wa ushiriki na upatikanaji wa fursa.**
Shinikizo la familia, Umaskini, ukosefu wa machaguzi, rasilimali chache, ukosefu wa wanawake walio mifano ya kuigwa yote yanachangia katika kutoshiriki na idadi kubwa ya wanaocha michezo.

**Uwakilishi mdogo katika nafasi za** uongozi.
Mawazo potofu ya jinsia katika michezo bado yanawaweka wanawake katika nafasi za utegemezi na kuwanyima uwezo.

**Vurugu na mazingira ya michezo yasiyo salama** yanachangia katika uzoefu wa kiwewe, matatizo ya ugonjwa wa afya ya akil na kukosekana kwa fursa kwa wanawake na wasichana.

**Ukosefu wa muda.**
Viwango vikubwa vya kazi zisizo na malipo na gharama za malezi ya Watoto zinawafanya wanawake na wasichana kuwa na uwakilishi mdogo kama washiriki katika nafasi zingine katika michezo.

**Katika nchi nyingi za Afrika imani potofu kuhusu jinsia, muingiliano, na mgawanyo wa majukumu.** Mtazamo wa kijinsia wa mgawanyo wa majukumu nyumbani unazuia ushiriki wa wanawake katika shughuli za burudani kama vile michezo. Wanawake wana muda kidogo wa kushiriki katika shughuli za michezo au burudani wanapotumia karibu 55% ya kazi yao ya jumla katika kazi isiyo na malipo, ikilinganishwa na 19% kwa wanaume. Hata wakati wanawake wanapoingia katika nguvukazi, wanakumbana na tofauti kubwa la malipo ya kijinsia. Tofauti ya kijinsia inaweza kuonekana, kwa mfano, timu za taifa za wanawake za mpira wa miguu, ambapo wanaweza kupata kidogo kama 1-5% ya nyongeza wanazopata wenzao wanaume. Wanawake wamekuwa katika michezo ya kujifurahisha au yenye malipo madogo, ambapo hujitolea kwa kiasi kikubwa, kama vile kuchukua likizo isiyo na malipo, kuacha kazi zao au kuacha masomo yao ili kushindana katika ngazi ya juu zaidi.

**Ukatili wa kingono na kijinsia ni moja ya masuala muhimu yanayozikumba jamii za Kiafrika. Ukatili wa kingono na kijinsia** hutokea kwasababu ya matarajio ya jamii yanayohusiana na jinsia, na vilevile tofauti kati ya wanawake na wanaume. Kote Afrika, wanawake na wasichana ambao ni wahanga wa ukatili nyumbani na katika maeneo ya umma hawana ulinzi wa kutosha katika michezo.

**Wanawake wana uwakilishi mdogo katika nafasi za uongozi.** chini ya 20% ya wanawake wanaotumikia katika vyombo vya serikali au bodi za vyama vya michezo. Njia za maendeleo kutoka kucheza hadi uongozi ni ndogo kwa kuwa wanawake na wasichana wanaendelea kukumbana na hatari ya kuingiza salama katika michezo.

**Kama huwezi kuiona, huwezi kuiga.** uwakilishi wa wanawake katika michezo ni mdogo katika nafasi zote, kama wanamichezo, makocha, waamuzi, wafanyakazi, na watazamaji katika michezo yote. Kama wanawake hawaonekani, hawawezi kuwahamisha wengine. Matokeo yake, huu ukosefu wa uwakilishi una athari hasi katika ushiriki wa wanawake na wasichana katika shughuli za michezo (kwa maendeleo), ambao hawana watu wa kuigwa.

**Vikwazo vikuu vya ushiriki katika michezo kwa wanawake na wasichana ni imani na mitazamo, vikwazo vya kiutamaduni, vikwazo vya kiuchumi, kukosekana kwa muda wa burudani, na upatikanaji mdogo wa vifaa na maeneo salama**

# MUELEKEO WA AUSC KUFIKIA USAWA WA KIJINSIA

Mtazamo wa tofauti ya usawa wa kijinsia katika michezo unaanzia kutoka katika ukweli kuwa wanawake kimsingi wanachukua nafasi binafsi au za ndani kama walezi wa msingi. Nafasi hiyo ya kubainisha nafasi jinsia huelekeza kaida za jamii na taratibu za kiutamaduni katika jamii na katika mazingira ya michezo.

Itifaki ya Maputo (ilipitishwa mwaka 2003) na Mkakati wa AU wa Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake ni nyaraka zinazoongoza ambazo zinatoa taarifa ya Ajenda ya AU. Kuanisha na kuingiza hii misimamo na mikakati ya usawa wa kijinsia kikanda na kitaifa ni muhimu ili kuchukuliwa hatua ya pamoja na jamii ya michezo.

Baraza la Michezo la AU ni muhimu katika utekelezaji wa Ajenda ya AU 2063, hususani Matamanio ya 6: "Afrika ambayo maendeleo yake yanasukumwa na watu, ikitegemea uwezo wa watu wa Afrika, hasa wanawake na vijana wake, na kuwalea watoto". Hii inaendana na Sheria ya Baraza la Michezo la AU kuhamasisha, kutetea na kulinda utamaduni wa usawa wa kijinsia katika uwanja wa michezo (Ibara ya 5) na lengo kuu la Sera ya AU la Maendeleo Endelevu ya Michezo Afrika, ambayo yanahamasisha Mataifa Wanachama, kanda za AUSC na mashirikisho ya michezo kuandaa na kuingiza usawa wa kijinsia, na mifumo ya sera salama na jumuishi kuwawezesha wasichana na wanawake. Kwa kuendeleza mamlaka ya Pamoja ya michezo na Michezo kwa Maendeleo (SfD), Baraza la AU la Michezo linatoa mwelekeo kwa serikali na watunga sera Afrika kuzingatia maendeleo na utekelezaji wa sera na taratibu zinazozingatia masuala ya jinsia.

# USAWA WA KIJINSIA KUPITIA MICHEZO

Kupitia michezo, wanawake na wasichana wanapata sehemu salama, wanajiheshimu, wanaimarika na kujifunza namna ya kutumia sauti zao – vipengele vyote muhimu vya kuwapatia ukombozi na uhuru.

Michezo inaonyesha uimara, uwezo na uwezeshaji wa wanawake na wasichana. Inawapatia jukwaa la umma kutoa changamoto kwa imani za kiutamaduni, wakati wakibadili mfumo wa alama wa maeneo ya umma na kutambua haki na mafanikio ya wanawake. Michezo pia ni kuhusu kulinda na kwa makusudi kuandaa sehemu salama ambazo zinakuza majadiliano makali kuhusu masuala ya haki za ngono, kuchukua hatua ya hatari na uwakala wa binadamu. Kwa kuwashirikisha wanaume na wavulana, , SfD wanaamsha ufahamu wa masuala ya usawa wa kijinsia na kusisitiza nafasi muhimu ambayo wanaume wanayopaswa kuchukua kama washirika na mifano ya kuigwa ya uanaume chanya katika jamii zao. Watu maaruku katika michezo, walimu walifundishwa vizuri, makocha na vijana viongozi ni mabalozi wa mabadiliko katika jamii vumilivu zaidi yenye usawa wa kijinsia. Familia, utamaduni, vyombo vya habari vya umma na jamii za michezo zinaelekeza utambulisho wa kijinsia katika njia mbalimbali. Wanariadha maarufu wa kike wanaweza kuwa na ushawishi mkubwa katika jamii na wanawashawishi wasichana duniani. Wanawake wa kuigwa wana nafasi muhimu kuchukua katika kubadili mawazo potofu na mitazamo mibovu ya kijinsia.

**Programu na shughuli za michezo zinatakiwa kuzingatia mazingira na juhudi, zinaakisi umiliki na kuhakikisha kunakuwa na ushirikishaji, usalama na matokeo sawa ya kijinsia.**



“Ni jukumu la pamoja la wadau wote kuhakikisha kuwa wanawake na wasichana wanapata fursa sawa katika michezo, na kuweka mazingira ambapo wanajihisi kuwa salama, kuwezeshwa, na kuandaliwa ipasavyo kuendelea na taaluma katika michezo.”

**Bi. Prudence Nonkululeko Ngwenya**
Mkurugenzi wa Wanawake, Jinsia na Vijana
Tume ya Umoja wa Afrika

# TARATIBU ZILIZO BORA

Nchini **Senegal**, wasichana na wanawake wengi wanakabiliwa na ukosefu wa habari kuhusu mzunguko wao wa hedhi na upatikanaji wa bidhaa za usafi; Katika utafiti uliofanywa na shirika la Speak-up Africa, asilimia 84 ya wasichana walisema kuwa hawakuhisi kujiandaa vya kutosha kipindi cha hedhi yao ya kwanza. Uelewa huu mdogo unadhuru afya zao, elimu, ushiriki wao katika michezo, na maisha yao ya kitaaluma na kijamii kwa ujumla. Ili kukabiliana na changamoto hizi, ApiAfrique, shirika la biashara ya kijamii kutoka Senegal iliyoanzishwa mwaka 2017 kwa lengo la kupunguza taka, kuhifadhi afya, na kukuza uwezeshaji wa wanawake, inaunda bidhaa na zana za kusaidia usimamizi wa hedhi salama (menstrual hygiene management- MHM). Kama sehemu ya mafunzo yao ya ufahamu kwa wanawake (vijana), familia zao, na (vijana) wanaume, ApiAfrique pia hutumia nyezo ya michezo kwa maendeleo (SfD). Kupitia mafunzo ya SfD, vijana wa kike hupata uelewa bora wa miili yao, kujihisi vizuri zaidi na miili yao, na kupokea taarifa na bidhaa wanazohitaji ili kudhibiti vizuri hedhi zao. Kwa kuhusisha (vijana) wanaume katika programu, ApiAfrique inalenga kubadilisha tamaduni za hedhi nchini Senegal.

Huko Kilifi, mji wa pwani **Kenya**, wasichana na vijana wa kike walio katika hali duni wanakumbwa na changamoto za mimba za utotoni, upatikanaji mdogo wa huduma za afya, viwango vya chini vya elimu na mifumo mibaya ya kijinsia. Tangia kuanzishwa kwa shirika la Moving the Goalposts (MTG) mnamo mwaka wa 2001, shirika hilo la kijamii limefikia wasichana na vijana wa kike zaidi ya 50,000, wenye umri wa kati ya miaka 9 hadi 25, na kuwapatia maarifa, ujuzi na fursa kupitia mpira wa miguu. MTG inatoa programu kadhaa, ikiwa ni pamoja na huduma za taarifa kuhusu haki na afya ya uzazi wakati wa mashindano mpira wa miguu. Aidha, shirika hilo linatumia ligi kama njia salama katika upatikanaji wa ajira, pamoja na fursa kwa washiriki kumaliza elimu zao na kuweza kujikimu kimaisha. Vijana wa kike pia wanapata mafunzo ya uongozi na ajira, na kunufaika na nafasi za kazi. MTG inatumia mbinu jumuishi kwa jamii, ikilenga kutoa maeneo salama na kubadilisha mitazamo hasi ya kijinsia.



# WITO WA KUCHUKUA HATUA

## AU INAPEWA WITO WA:

- Kuboresha na kuoanisha sera za michezo na Michezo kwa Maendeleo, ili kutoa mwongozo na kufuatilia uanishaji wa sera za taifa na kanda na taratibu ambazo zinachangia katika ajenda ya pamoja ya kuendeleza usawa wa kijinsia.
- Kushiriki katika mkakati wa utetezi, utafutaji wa rasilimali na uhamasishajiwa usawa wa kijinsia ndani ya sekta za michezo na Michezo kwa Maendeleo.
- Kukuza falsafa na programu za usawa ya kijinsia ili kuziba pengo kati ya ushindani katika michezo na Michezo kwa Maendeleo.
- Kukuza usawa wa kijinsia katika Michezo ya Afrika kwa kusisitiza katika usawa wa matukio yanayoenda Pamoja na kuwapa moyo wanariadha wa Afrika kutetea haki ya kijinsia.
- Kufanya maamuzi ya sera ambazo zinahimiza Nchi Wanachama kuingiza na kutambua Michezo kwa Maendeleo na kuingiza katika sera, mikakati na bajeti zao za michezo ya taifa.

## NCHI WANACHAMA WA AU ZINAPASWA:

- Kuandaa mfumo wa sera ambao unaingiza usawa wa kijinsia, michezo salama na shirikishi.
- Kujenga uwezo endelevu wa, kifedha na kitaasisi kutekeleza misimamo ya kimataifa, kibara, kikanda na kitaifa ya kupanga mipango, bajeti, programu na utafiti wa maendeleo ya michezo na Michezo kwa Maendeleo kwa kuzingatia masuala ya jinsia.
- Ushirikiano na wadau mbalimbali kuendeleza ajenda ya pamoja ya kitaifa ya usawa wa kijinsia na kuangalia shughuli na rasilimali zinazojirudia kutokana na mifumo mbalimbali ya utekelezaji ndani ya serikali na sekta.
- Kukuza kimkakati, kugharimia na kuweka malengo ya usawa wa kijinsia katika maandalizi ya michezo, ufundishaji, nafasi za kitaalamu na uongozi, wakati wa kutekeleza adhabu kwa kutofuata sera na sheria.
- Kujenga mazingira yanayowezesha michezo kwa kuhakikisha ushiriki salama, ulinzi na haki za binadamu na uhuru katika ngazi zote kwa kusisitiza utekelezaji wa sera za ulinzi katika michezo.

## SEKTA YA BIASHARA INAPASWA:

- Kushirikiana na wakala wa michezo kubadilishana muundo wa biashara na kuchangia katika kuingiza utaalamu katika sekta ya michezo kwa kujenga uongozi, umiliki na ujasiriamali kwa wanawake.
- Kufadhili wanamichezo wa kike na michezo ya wanawake ya hadhi ya juu, na piakukuza usawa wa kijinsia katika utangazaji na mawasiliano.
- Kujitolea katika uwezeshaji wa kijamii na kiuchumi wa wasichana wadogo kwa kutoa ufadhili, mafunzo yanayozingatia kazi na fursa za kazi.
- Kutoa na kufuatilia fedha za uwekezaji wa shirika katika Jamii kufadhili mashirika ya kijamii ili kuwezesha wanawake na wasichana katika jitihada za michezo na Michezo kwa Maendeleo.

## VYOMBO VYA HABARI VINAPASWA:

- Kuongeza kiwango cha kuonekana kwa wanawake na wasichana katika michezo kwa kutoa muda zaidi wa matangazo/nafasi kuwavutia wafadhili na umma.
- Kuajiri waandishi wa habari wa kike na kukuza utaratibu wa kutoa ripoti zinaozingatia jinsia na kuondoa Mawazo potofu.
- Kuchapisha/kutoa habari za wanamchezowa kike wenye mafanikio ambao wamevuka vikwazo na changamoto mbalimbali kufika kileleni.

## ASASI ZA KIRAIA ZINAPASWA:

- Kujenga ushirikiano na taasisi zingine zinazolingana, serikali, washirika wa maendeleo ili kutetea kwa pamoja upatikanaji endelevu wa fedha na rasilimali kutekeleza programu za maendeleo ya kijinsia katika michezo na Michezo kwa Maendeleo.
- Kushiriki katika njia za kibunifu na kutumia michezo kama kichocheo kufikia na kushughulikia mahitaji ya wanawake wengi walio katika mazingira magumu (k.m. wakimbizi, kina mama vijana, jamii za vijijini na watu wenye ulemavu).

# MAREJEO YA TAARIFA


World Economic Forum (2022). Global Gender Gap Report 2022. Inapatikana: https://www.weforum.org/reports/global-gender-gap-report-2022

AU Gender Policy (2018-2028). Inapatikana: https://au.int/sites/default/files/documents/36195-doc-au_strategy_for_gender_equality_womens_empowerment_2018-2028_report.pdf

UNESCO. Gender equality and education. Inapatikana: https://www.unesco.org/en/gender-equality/education

GIZ (2018). Implementing development goals: Sport and gender equality. Inapatikana: https://www.sport-for-development.com/imglib/downloads/giz2018-en-Implementing-development-goals-sport-for-gender-equality.pdf

ApiAfrique. Inapatikana: https://apiafrique.com/

Moving The Goalposts (MTG). Inapatikana: https://mtgk.org/programs



**MAWASILIANO:**


https://sportscouncil.au.int
AUSC@africa-union.org

African Union Sports Council
B.P.: 1363,
Yaoundé, Cameroon
Rue No. 1798, Bastos No 192



© GIZ/EAC Madola Grafix (ukurasa 1)
© African Union Commission (ukurasa 3)
©TYSA (ukurasa 5)
© GIZ/Tina Krueger (ukurasa 8)

Haki miliki © African Union Sports Council, 2024. Haki zote zimehifadhiwa